**THE MATHEMATICAL ASSOCIATION OF TANZANIA**
**(Chama cha Hisabati Tanzania)**
**MAT/CHAHITA**

MATHEMATICAL ASSOCIATION OF TANZANIA
SINCE 1966
CHAMA CHA HISABATI TANZANIA

**MAT/CHAHITA**
**Department of Mathematics - University of Dar es Salaam**
**Mobile: +255 745 626 665/0689 561 555**
**Website:** http://chahita.or.tz/
**P. O. Box 35062,**
**DAR ES SALAAM.**

**Our Ref:** MAT/IDM/2024 **09 /03/2024**

---

## MAT/CHAHITA - MAADHIMISHO YA SIKU YA HISABATI DUNIANI (INTERNATIONAL DAY OF MATHEMATICS - IDM) 2024

Kwa mara nyingine tena tutakuwa na Maadhimisho ya Siku ya Hisabati Duniani (IDM), 2024. Kilele cha maadhimisho kitakuwa ni tarehe 14/03/2024 na kitaifa yatafanyika katika manispaa ya Morogoro, Uwanja wa Jamhuri. MAT/CHAHITA kwa kushirikiana na; TESP Mathematics Center ya Chuo Cha Ualimu Cha Morogoro (MOTCO) na Idara ya Hisabati, UDSM, wataratibu maadhimisho haya. Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda. Maadhimisho haya yatatumika ikiwa ni sehemu ya kuhamamisha, kujitathmini na kuweka mikakati katika kupambana na changamoto za somo la Hisabati.

Kauli Mbiu: **CHEZA NA HISABATI**
**Maelezo zaidi tembelea: https://www.idm314.org/**

Tunawakaribisha wote siku ya kilele katika Manispaa ya Morogoro na wengine kadiri mtakavyoweza/wezeshwa.

Maadhimisho haya pia hutanguliwa na shughuli ya wiki moja ya kujitolea kufundisha na pia kuhamasisha na kuwapa hamasa na motisha walimu na wanafunzi kupenda na kujifunza Hisabati na Sayansi katika shule mbalimbali. Mara hii shughuli hii imefanyika mkoa wa Dar es Salaam katika shule tatu za sekondari. Wiki hii ni kuanzia 04 hadi 08/03/2024.

Hivyo ni vizuri kujua kuwa mafanikio ya somo la Hisabati Tanzania yanahitaji juhudi za pamoja za wadau mbalimbali ikihusisha:



CamScanner

**Wanafunzi**: Hawa ndiyo wateja wetu mahsusi. Wawe na **UTAYARI** kwa kufanya juhudi katika kusoma, kutenga na kujilazimisha kufanya mazoezi ili kujenga uelewa wa Hisabati. Kujenga ushirikiano baina yao katika kufikia mafanikio ya kielimu, kuanzisha na kushiriki shughuli za club za Hisabati, nk. Pia watambue kuwa wao wanaandaliwa maisha yao, hivyo wafanye juhudi za kutosha katika kuyaandaa maisha yao kwa kuzingatia wazazi au walezi ni wa muda tuu.

**Wazazi/Walezi:** Kuwatia moyo watoto/wanafunzi ili wapende Hisabati, kuwasimamia kuhakikisha wanasoma na kufanya majaribio au mazoezi wanayopewa shuleni. Kuondoa kabisa mitizamo na dhana za kukatisha tamaa kuwa Hisabati ni ngumu. Wajenge ushirikiano na walimu katika kuwaandaa wanafunzi.

**Walimu**: Kufundisha kwa **moyo wa UPENDO** na **TABASAMU** somo la Hisabati, na pia kuwa **rafiki wa kitaaluma** kwa wanafunzi. Kutumia zana rahisi za ufundishaji Hisabati kulingana na mazingira. Kuwa na **UBUNIFU** na **UVUMBUZ**I katika ufundishaji na ujifunzaji. Kujenga ushirikiano baina yenu katika ufundishaji. Hili ni Somo rahisi sana hasa likifundishwa kwa kuhusisha na matumizi halisia wa maisha ya kila siku katika jamii na pia kutumia zana rahisi.

**Wadau Mbalimbali:** Wabunge, NGOs zote tunaomba zishiriki kuhamasisha, kuwezesha na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuelimisha na pia kukosoa masuala yanayodidimiza Hisabati mashuleni. Mfano Programu ya KIUHISABATI katika Jimbo la Ubungo, Dar es Salaam imeendelea kusaidia sana walimu na wanafunzi kuweza kufanya juhudi na kuongeza ufaulu wa Hisabati katika matokeo ya kidato cha nne ya mitihani iliyofanyika 2021 na 2022. Juhudi za mradi wa serikali wa TESP wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa walimu wa Hisabati wa shule za msingi, sekondari, na vyuo vya Ualimu umeonesha mafanikio katika Halmashauri na vyuo husika. Pia mradi mpya wa SEQUIP umeweza kufanyika vizuri nchi nzima na umeongeza ufanisi zaidi. Matokeo ya mitihani ya kidato cha 4 ya 2023 yaliyotangzwa Jnuari 2024, ufaulu wa Hisabati umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 5, kutoka 20.08% hadi 25.42%. Hili ongezeko ambalo limechukua Zaidi ya miaka 15, tangu 2008. Hii itakuwa imechangiwa na juhudi za mradi wa SEQUIP pamoja miradi mingine ya Wadau.

**Serikali**: Imeendelea kuimarisha miundombinu kwa kiasi kikubwa hasa ujenzi wa madarasa katika shule. Tunatoa pongezi za kutosha na kuwaomba wasimamizi kuilinda miundombinu hii.Pia tunaipongeza serikali kwa kuendelea na jitihada za kuondoa maswali ya kuchagua katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi.

**Wito wetu kwa serikali**:

Kuhakikisha walimu wanaajiriwa wa kutosha, kuboresha maslahi kulingana na mzigo wa ufundisha kwa walimu wa Hisabati. Kuongeza vitabu na nyenzo za ufundishaji na kuhakikisha zinafika katika kila shule na hasa za vijijini. Ni humu sana shule hizi ambako kwa ujumla ufaulu wa shule huwa ni wa chini kidogo ukilinganisha na shule za mijini.

Pia Kufanya zaidi tathmini na utafiti wa matokeo ya mitihani ya kitaifa kwa kushirikiana na MAT/CHAHITA na Wadau wengine ili kuweka mikakati ya kuboresha zaidi. Mfano ufaulu wa mitihani ya kidato cha nne 2023, Hisabati ina 25.42% (kutoka 20.08% - 2022) na somo linalofuata ni Historia yenye ufaulu wa 63.2%. Hivyo kuna haja ya kuwa na juhudi maalum



CamScanner

katika somo hili kama taifa ili kulikwamua. Ikumbukwe kuwa katika kumbukumbu za ufaulu wa kitaifa wa kidato cha nne katika miaka ya 1972 na 1976 wastani ilikuwa 39.22% na pia mwaka 1975 ufaulu ulikuwa ni wa juu kwa 52%. Hitajio la ufaulu wa Dunia kwa mujibu wa benki ya Dunia ni kuanzia 31%. Hivyo tunahitaji mikakati imara ili kuweza kusonga mbele kwa lengo la kusaidia taifa letu.

Pia tunaiomba serikali isaidie kutuunganisha kupitia vikao vya pamoja na asasi mbalimbali zenye miradi ya Hisabati ili kujadiliana ni namna gani wamefanikiwa katika miradi yao katika kulikwamua somo la Hisabati ili kuunganisha nguvu ya kitaifa katika kuongeza ufanisi na tija.

**Matarajio yajayo:**

- Kuweza kuongeza juhudi katika kufundisha na kujifunza Hisabati huku tukijenga ushirikiano zaidi na kufuatilia maudhui ya mtaala mpya.
- Kila mkoa kupitia halmashauri zake waanzishe zawadi maalum kwa halmashauri inayoongoza kufaulisha Hisabati kwa walimu wake. Hii italeta hamasa na ushindani kwa kila halmashauri. Tunaomba hii ifanyike kwa Tanzania Bara na Visiwani ikiwa ni pamoja na kuweza kufanya shughuli za Hisabati mfano, maonesho kwa wanafunzi, mitihani mbalmbali na zawadi kwa wanafunzi ili kuwapa Motisha, Upendo na Hamasa katika somo la Hisabati.
- Kuongeza vifaa na elimu ya TEHAMA katika shule zetu ili kupunguza baadhi ya changamoto na kuendana na hitajio la ulimwengu kwa sasa.

**MSISITIZO KWA WOTE:**

Huu ni ujenzi wa Taifa letu, hivyo tuendelee kupambana kwa maendeleo endelevu katika kuunga mkono juhudi za Serikali ya awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dr Samia Saluhu Hassan.

Wito wangu ni kila mkoa, Wilaya/Halmashauri, Kata au Shule kuweza kuadhimisha kwa mfano wa shughuli hizi za kitaifa na zaidi kufanya kutathmini na kutafakari juu ya ufaulu wa somo letu ambapo kwa mfano wastani wa Ufaulu ni 25.42% kwa Kidato cha nne, je shule yako ina wastani gani? Ufaulu wa 25.42% wa 2023, shule yako ina wastani gani na wapi tunakwama na mbinu za kujikwamua. Pamoja na changamoto zilizopo, tujipange tuwe sehemu ya suluhisho.

**NAWATAKIA KILA LA KHERI KATIKA MAADHIMISHO YA IDM 2024 NA MWENYEZI MUNGU ATUBARIKI WOTE**

**Imeandaliwa na Dkt. Said Sima – Mwenyekiti, MAT/CHAHITA**



CamScanner